

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA HAMSINI**

21 JUNI, 2019



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI – TAREHE 21 JUNI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

421. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA  
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kuwa Watumishi hewa hawapo katika “payroll” ya Serikali:-

Je, Serikali inadhhibiti vipi mishahara ya Watumishi wasiostahili kulipwa kama Wastaafu, Waliofariki, Walioacha kazi na Waliofukuzwa kazi katika Halmashauri.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**422. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN  
GHASIA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,  
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha  
kuwa Hospitali ya Mkoa wa Mtwara Ligula  
inapata Madaktari Bingwa wa kutosha.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**423. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, na  
Biashara:- Mazingira ya kufanya biashara nchini  
ni magumu na hii ni kwa Wafanyabishara wa  
ndani na wa nje:-

Je, ni lini Serikali itaondoa urasimu ili Wananchi  
waweze kunufaika.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **424. MHESHIMIWA KITETO ZAWADI KOSHUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Ili kuelekea Tanzania ya Viwanda, Watanzania wanapaswa kuandaliwa vema ili kushiriki kikamilifu katika Viwanda vya ndani:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuandaa Wataalamu mbalimbali watakaotumika katika kuendesha Viwanda nchini.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **425. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Magari mengi ya Serikali yanafanyiwa *Service* kwenye gereji kubwa hapa nchini lakini hii imekuwa tofauti kwa magari yanayomilikiwa na Jeshi la Polisi:-

Je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu wa kuwa na maeneo ya kutengeneza na kurekebisha magari ya Polisi ili kuliimarishia vitendea kazi.

**426. MHESHIMIWA JUSTIN JOSEPH MONKO  
(SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na changamoto za kiusalama katika Jimbo la Singida Kaskazini kutokana na jiografia yake na rasilimali zilizopo:-

Je, ni lini Serikali itaongeza Vituo vya Polisi katika Kata za Mughunga, Mgori na Merya ili kuimarisha usalama wa Wananchi na mali zao.

**427. MHESHIMIWA DKT. RASHID MOHAMED  
CHUACHUA (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mwaka 2017/2018 kulitokea mauaji ya Vijana wa bodaboda katika Wilaya ya Masasi ambapo Vijana wanaokaribia kuwa zaidi ya kumi wameuwawa kikatili na kunyang'anywa pikipiki:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu matukio haya katika Wilaya ya Masasi.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**428. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Mfumo wa *Vehicle Tracking System (VTS)* umefungwa katika mabasi yote nchini ili kudhibiti mwendokasi kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani:-

- (a) Je, mfumo huo umegharimu fedha kiasi gani;
- (b) Je, Mzabuni wa kazi hii kwanini hakupatikana kwa ushindani kwa kufuata Sheria ya Manunuzi;
- (c) Je, mfumo huu unaendeshwa na kusimamiwa na nani.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**429. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wananchi wa Wilaya ya Itilima Mkoani Simiyu huvamiwa na kuharibiwa mazao yao na

Wanyama aina ya Tembo na Serikali hutoa fidia kidogo na wakati mwingine kutowafidia kabisa:-

Je, Serikali inatoa ahadi gani kwa Wakulima juu ya fidia kwa waathirika wa uvamizi huo.

**430. MHESHIMIWA MBAROUK SALIM ALI (WETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni mafanikio gani yameweza kupatikana katika kushirikisha jamii katika jitihada za usimamizi wa maliasili nchini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**431. MHESHIMIWA ALLY SEIF UGANDO (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Jimbo la Kibiti lina Kata 5 na Vijiji 17, sawa na Vitongoji 72 ambavyo vipo kwenye maeneo ya Delta lakini havina umeme:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme kwenye visiwa hivyo;
- (b) Je, utapelekwa umeme wa aina gani.

**432. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWEKI KIWANGA (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kata za Mchombe, Igima, Mbingu, Namwawala na Idete katika Jimbo la Mlimba zilipelekewa mradi wa umeme kwa gharama nafuu lakini mradi huo umefanywa vibaya na hivyo kusababisha Wananchi wengi kukosa umeme:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwa Wananchi hao;

(b) REA ilimkabidhi Mkandarasi kupima maeneo yatakayounganishwa umeme katika Vijiji vya Msolwa, Miembeni, Iduimdembo, Ipungusa, Matema, Lumumwe, Uchindile, Kitete na Ngwasi katika Awamu ya Pili; Je, kwa nini kazi hiyo inasuasua.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**433. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-



Je, Serikali inasema nini kuhusu ucheleweshaji wa kupata hati za kumiliki ardhi.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
21 JUNI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**

**IV. KAULI ZA MAWAZIRI:**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:**